



Mabadiliko ya Serikali Mkakati Inawezekana



Wacha uchafuzi wa [CCM](#) Jumatano 29 Oct 2025 upite. Siku ya uchafuzi
⇒ maandamano ya amani na usafi wa mazingira ⇒ wajichague wenyewe
[Serikali](#) ikwapue madaraka ikijua fika kabisa haikubaliki hata punje na
wananchi kwa wingi wetu wote. Umma unawakataa. Hatuwataki

[1] Serikari ijue haina **ridhaa** ⇒ wajiongoze wenyewe

- Uchafuzi ugomewe. Kama lazima uonekane, haribu kura. Watashinda. Goli la Mkono. Watachakachua. Tutaona namba zitakazotoka [INEC](#) / [ZEC](#)
- Kutoshiriki uapishwaji. Waende mabalozi tu na wanajeshi (wameapa)
- 9 Dec Siku ya Usafi wa Mazingira - II (kama serikali dhalimu bado itakuwepo)

[2] Baada tu ya kuapishwa, watanganyika **kugoma** kuongozwa na hao watekaji, walafi, malimbukeni, wala rushwa, [wanafiki](#), walevi wa madaraka, [ndumilakuwili](#), wasiojua [demokrasia](#), vilaza

- Tusikubali kutawaliwa. Nchi nzima Tugome, Tususe, [Tuzire](#); hata vibaka na majambazi chukueni likizo. Wanaobaki kazini wawe madaktari na wauguzi tu. Shughuli zote zisimame. Hawawezi kutulazimisha. Hawawezi kutushurutisha. Hawawezi kututeka wote. Tunaweza ([Nyerere](#), [Gandhi](#), [Mandela](#), [Islam](#), [Luther King](#)) Serikali [dhaifu](#) haidumu

Tukatae kata kata kutawalika. Tunagoma, Tunasusa, Tunazira. Nia na lengo ni kusimamisha shughuli zote hususan za kiuchumi. Hakuna simba wala yanga, hakuna twanga wala pepeta, hata harusi zihairishwe. Maandamano pekee hayatawang'oa. Dawa ni wote **kugoma** - walimu, wanafunzi, maofisa, madereva, mama lishe, machinga, ...

Silaha yetu ni wingi na umoja wetu. Tutabaki majumbani mwetu na mitaani kwetu tule ugali wetu mpaka watoke. Inatupasa kujitoa mhanga na kusaidiana. Tutavuka

Jumatano, 29 Oct 2025 Siku ya Usafi wa Mazingira

#UsafiOyee #MazingiraOyee #SamiaMustGo



[Majaji](#) mnatuangusha - simameni. [Wanahabari](#) mnatuangusha - simameni. [Wasanii](#) mnatuangusha - simameni. [Polisi](#) mnatuangusha - simameni. [Wanazuoni](#) mnatuangusha - simameni. [Wanasheria](#) jitokezeni maradufu. Makasisi [1], [2], [3], [4], ... (sio wajasiliamali, matapeli) mnatuangusha - simameni. [Wabunge](#) mnatuangusha - simameni. Wanauchumi [1], [2], [3], [4], [5], ... mnatuangusha - simameni, [Walimu](#) mnatuangusha - simameni. [Wanadiplomasia](#) mnatuangusha - simameni. [Uhamiaji](#) kaeni chonjo - wasitoroke. Magereza jiandaeni - neema tele inakuja



Ndugu jirani mtekaji, usiyejulikana, kibaraka, msaliti, mtesi, mamuluki, uliyemwaga risasi Dodoma unatuangusha - simama. Jitete. Kata minyororo ya utumwa. Sitisha ukaragosi. Usiuze **utu** wako kwa vipande thelathini. Punguzo la adhabu lipo. Rudisha dhamira safi. Rekebisha dira. Tubu wakati muda bado unao. Utakimbilia wapi? Umati kwa mawe na marungu wanaijia nafsi yako. Jiokoe sasa



Matakwa yetu ni wazi

- ⇒ Serikali ya Samia Ijiuzulu. Lini? Jana (neni maridhiano / muafaka ni najisi)
- ⇒ Baraza la mpito
- ⇒ Katiba mpya (muungano, tume huria, uhuru wa habari na mawasiliano, ...)
- ⇒ Kufutwa kwa kesi zote za kubambikiwa na za kisiasa (mnamuonea)
- ⇒ Haki kwa walioteswa, kupotea, kupoteza uhai (walizaliwa na Mama)
- ⇒ Haki kwa uchumi wetu unaojisiwa (ufisadi, kukolonishwa tena, ukaburu ...)

Kazi kubwa inatusubiri. Hii nayo inaelekeza maandamano yawe ya amani. Hatuhitaji fujo, vurugu, moto, uharibifu, ... Tushikamane. Tusaidiane. Kwa utulivu tutavuka. Maandamano ni mteremko, mabadiliko sahihi ni mlima



[JWTZ](#) lindeni mipaka ya nchi. Tunawashukuru kwa uzalendo wenu. Mabadiliko haya ni Jihad yetu sisi raia. Hatukwepi jukumu letu. Tunabeba msalaba huu. Hili hatulifanyii mzaha, utani wala masihara. Hatuchezi kamali na jeshi. Bila kigugumizi wala kumung'unya maneno - Wanajeshi bakini makambini. Tunawaheshimu. Tunawapenda

Jumatano, 29 Oct 2025 Siku ya Usafi wa Mazingira

#UsafiOyee #MazingiraOyee #SamiaMustGo